HALMASHAURI YA WILAYA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI IFWAGI,

S.L.P.117,

MAFINGA.

18/12/2020

KUMB. Na. IFWSS/VOL. I/…….

MWANAFUNZI_____

S.L.P_____

_____

YAH. <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IFWAGI WILAYA YA MUFINDI MWAKA 2021</u>

1.0. Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika SHULE HII kwa mwaka 2021. Shule ya sekondari Ifwagi ipo umbali wa kilometa 20 Mashariki mwa mji wa Mafinga. Usafiri wa basi kutoka Mafinga unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mafinga, nauli Tshs. 3,000/= kwa basi na Tshs. 4,000/= kwa Taxi au Noah. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021.

1.1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.2. SARE ZA SHULE.

a) Wasichana

- **i.** Sketi mbili za rangi ya kijani ndefu zinazoishia **kwenye kifundo cha mguu ziwe na marinda manne na rinda boksi mbili mbele na nyuma.**
- **ii.** Blauzi nyeupe mbili mikono mirefu.
- **iii.** Brazia nyeupe mbili, haturuhusu nguo za ndani za rangi tofauti na shati la shule.
- **iv.** Tai ndefu ya rangi ya kijani.
- **v.** Viatu vya ngozi nyeusi jozi mbili vya kufunga na kamba visiwe buti na visiwe na kisigino kirefu.
- **vi.** Soksi nyeupe jozi mbili.
- **vii.** Sweta ya rangi ya kijani yenye shingo ya **V.**

NB: rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule kwa wanafunzi Waislam

b) WAVULANA

i. **Suruali mbili** za khaki Amerikani khaki zenye marinda mawili **zenye turn up upana mguuni chini iwe nchi 16-17.**
NB: ZINGATIA suruali zilizobanwa chini haziruhusiwi kabisa.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu, kaoshi au fulana mbili za rangi nyeupe. Nguo za ndani tofauti na nyeupe haziruhusiwi.
iii. Tai ndefu ya rangi ya kijani.
iv. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kufunga na kamba visiwe buti
v. Soksi nyeusi ndefu jozi mbili
vi. Sweta la rangi ya kijani lenye shingo ya **V.**

c) Sare za michezo kwa shule kwa mwaka huu, kwa wavulana raba, bukta na T-shirt vya rangi KIJANI na kwa wasichana; ni raba track suit ya rangi KIJANI.

2.2. Daftari za kutosha aina ya (**caunta book two quire)** kwa masomo kumi na moja, kalamu za kutosha na mkebe wa hesabu.

2. 3 kamusi ya kiingereza kwa kiingereza (**Oxford students dictionary**)

2.4 Rimu moja ya karatasi za kutolea **copy A4** kwa ajili ya mazoezi mbalimbali na awapo hapa shuleni.

CHAKULA SHULENI

Ili wanafunzi waweze kuzingatia masomo vizuri upo utaratibu wa kuchangia chakula unao simamiwa na kamati ya chakula na mchango huo ni kama ifuatavyo:

i. Mahindi kwa mwaka ni madebe matatu.
ii. Maharage kwa mwaka ni kilo 20 sawa na lita za maharage 20.
iii. Fedha taslimu 25,000/= kwa mwaka kwa ajili ya kuwalipa wapishi, kununulia mafuta ya kupikia, chumvi, gharama za mashine na matumizi madogomadogo.
NB: Maharage, mahindi, pamoja na fedha vyote vitakusanywa na kamati ya chakula inayoundwa na wajumbe wawakilishi wa wazazi kutoka vijiji vyote vyenye wanafunzi wanaosoma hapa shuleni.

VIFAA VYA USAFI

Kila mwanafunzi atapaswa kuja na fagio moja (chelewa) na ndoo ya lita kumi kwa ajili ya kumsaidia usafi.

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Raisi-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kufika shuleni.

1) KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

1. Ni lazima kuwaheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii nzima kwa ujumla.
2. Ni lazima kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na katika shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
3. Ni lazima kushiriki maandalio ya jioni (PREPARATION) ukiwa nyumbani au maeneo jirani na shule.
4. Ni lazima kuwahi kufika shule na katika shughuli nyingine yoyote utakayo pangiwa.
5. Ni lazima kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira muda wote uwapo shuleni.
7. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
8. Kutunza mali zako, za wenzio na mali za umma.

B. MAMBO USIYORUHUSIWA KUFANYA UKIWA MWANAFUNZI.

- Kutembelea maeneo yote ya starehe, vilabu vya pombe, nyumba za kulala wageni.
- Kufuga nywele, kusuka na kunyoa nywele katika mtindo wowote mfano pank, kiduku n.k
- Kufuga kucha, kupaka rangi kucha na kutumia vipodozi vya aina yoyote ile, poda, makeup na mafuta, pafyumu zenye harufu kali.
- Kuvaa mapambo ya aina yoyote ile mfano pete, mikufu, bangili za aina yoyote, heleni n.k.
- Kutembelea nyumba za walimu, ofisi ya mkuu wa shule, ofisi ya walimu maabara jikoni bila kibali maalumu.

C. MAKOSA YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.

1) Kutohudhuria vipindi vya masomo darasani
2) Wizi
3) Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
4) Ulevi wa pombe, kuuza au kutumia madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine mirungi, kubeli na kadhalika.
5) Kupiga au kupigana.
6) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7) Kudharau bendera ya Taifa.
8) Kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
9) Kuoa au kuolewa.
10) Kutoa mimba.
11) Kugoma adhabu halali, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
12) Kukataa adhabu kwa makusudi.
13) Kumiliki na kutumia simu ya mkononi wakatgi wote uwapo mwanafunzi.
14) Kufanya jaribio la kujiua.

4. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

- ✓ **Medical examination form** (fomu ya hospitali) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya au kituo cha afya cha serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
  - ✓ fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika
- ✓ Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sharia, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- ✓ Nakala ya cheti cha kuzaliwa

NB: tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana katika shule hii

_____

NASHON B NDANZI

MKUU WA SHULE.

KIAMBATANISHO **A**

SHULE YA SEKONDARI IFWAGI
S.L.P 117,
MAFINGA.
TAREHE……

DAKTARI_____,
HOSPITALI YA _____,
S.L.P _____

FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI

Tafadhali tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapa chini kwa gharama za mzazi/mlezi wake na uthibitishe kama ataweza kuendelea na masomo ya sekondari katika SHULE HII.
NI MUHIMU APIMWE KABLA YA KUJA SHULENI
JINA LA MWANAFUNZI _____

Matokeo ya vipimo vya afya ya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

1. Urine ……..
2. Stool ……...
3. HB……
4. Pregnancy ……
5. Spleen ……
6. Chest ……
7. Physical abnormality ……
8. …….
9. …….
10. ……

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu ……
ataweza/hawezi kuendelea na masomo ya sekondari.

…… …… ……..

JINA LA DAKTARI SAHIHI CHEO

MUHURI NA TAREHE …….

KIAMBATANISHO **C**

FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi…….. Jinsia……
Kabila …… tarehe kuzaliwa…… tarehe ya kuandikishwa shuleni / /2021.

2. Jina la baba…….
Je yu hai? Ndiyo au hapana……..
Kazi yake …….. anwani yake ……
Mahali anapoishi ……. Namba ya simu……..

3. Jina la mama ……
Je yu hai? ? Ndiyo ☐ au hapana ☐ weka tiki panapohusika
Kazi yake…… anwani yake ……
Mahali anapoishi ……. Namba ya simu……..

4. Jina la mlezi……..
Kazi yake …….. anwani yake ……
Mahali anapoishi ……. Namba ya simu……..

5. Ndugu wengine

JINA	UHUSIANO	NAMBA YA SIMU